and that I will serve it wholeheartedly and that I will defend
and protect the Constitution of Zanzibar and its people in
accordance with the established laws.

So help me God.

(2) OATH OF EXECUTION OF OFFICE OF REGIONAL/DISTRICT
ADMINISTRATIVE OFFICER

I
swear by Almighty God that I shall well and truly
solemnly and sincerely declare
serve Zanzibar in the execution of my duties as Regional/
District Administrative Officer, and shall at all times advise
the Regional/Area Commissioner in good faith and will not
directly or indirectly reveal the nature or contents of any
documents of the Revolutionary Government.

So help me God.

I hereby confirm that I have taken these Oaths at
..... Zanzibar, today day of
..... 19.....

.....
Signature

Sworn
Declared before me

the Regional Commissioner of

this day of 19.....

.....
REGIONAL COMMISSIONER

.....
REGION.

SCHEDULE TWO

APPOINTMENT AS

(UNDER SECTION 5)

TO

GREETINGS:

IN EXERCISE of the powers conferred upon me under
section of the Constitution, I APPOINT YOU

AS

with effect from day of 19.....

AND DIRECT YOU to do and exercise all powers of the

..... including other
powers which may conferred upon you from time to time in
accordance with the law in good faith and determination.

.....
PRESIDENT OF ZANZIBAR
AND
CHAIRMAN OF THE REVOLUTIONARY
COUNCIL, ZANZIBAR.

ZANZIBAR 19.....

25/....

- 25 -

IN WITNESS WHEREOF I have hereunto set my hand and
Seal of the Revolutionary Government of Zanzibar this

day of 19.....


PRESIDENT OF ZANZIBAR

AND

CHAIRMAN OF THE REVOLUTIONARY
COUNCIL, ZANZIBAR.

ZANZIBAR, 19.....

Passed in the House of Representatives on 21st
January, 1986.


Salum Mzee

SALUM MZEE

ACTING CLERK TO THE HOUSE OF
REPRESENTATIVES.

SHERTA YA KUWEKA VIAPO VYA UAMINIFU,
VIAPO VYA UTENDAJI KAZI, HATI ZA
UTEUZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA
NA VIAPO HIVI

Kifungu

1. Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Ufafamuzi.
3. Nani anaetakiwa kula kiapo cha Uaminifu.
4. Nani ataapisha viapo vya Uaminifu.
5. Hati za Uteuzi.
6. Kamuni.
7. Kuhalalalisha Viapo vilivyopita.

JADWELI NAMBA I

1. Kiapo cha Rais.
2. Kiapo cha Waziri Kiongozi.
3. Kiapo cha Majaji.
- 4A. Kiapo cha Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi.
- 4B. Kiapo cha Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ja Zanzibar.
5. Kiapo cha Naib Waziri.
6. Kiapo cha Mwanasheria Mkuu.
7. Kiapo cha Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.
8. Kiapo cha Spika wa Baraza la Wawakilishi.
9. Kiapo cha Katibu wa Baraza la Wawakilishi.
10. Kiapo cha Utekelezaji Kazi za Udhibiti wa Ukaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- 11A. Kiapo cha Katibu Mkuu/Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi.
- 11B. Kiapo cha Katibu/Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi.
12. Kiapo cha Mkuu wa Mkoa.
- 12B. Kiapo cha Mkuu wa Wilaya.
13. Kiapo cha Kadhi Mkuu.
14. Kiapo cha Utekelezaji Kazi za Mkuu wa Idara Maalum.
15. Kiapo cha Mshauri wa Rais.
16. Kiapo cha Katibu wa Rais.
17. Kiapo cha Utendaji Kazi cha Afisa Tawala Mkoa/Wilaya.

JADWELI NAMBA II

1. Uteuzi.

SHERIA NAM. 1 YA 1986

NAKURALI

Idris Abdul Salik

IDRIS ABDULWAKIL
RAIS WA ZANZIBAR
NA
MWENYEKITI WA
BARAZA LA MAPINDUZI

19 FEBRUARI 1986

SHERIA YA KUWEKA VIAPO VYA UAMINIFU,
VIAPO VYA UTENDAJI KAZI, HATI ZA
UTEUZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA
NA VIAPO HIVI

IMETUNGWA NA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.

Jina fupi
na tarehe
ya kuanza
kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kuwa ni sheria ya viapo
vya uaminifu na Hati za Uteuzi na itahesabiwa kwamba imeanza
kutumika tokea tarehe 1 Oktoba, 1985.

Ufafaruzi.
Ufahamu:-

"Mteuzi" ina maana ya mtu ye yote kwa mujibu
wa Katiba au sheria nyengine yo yote, mtu
huyo anatakiwa ateuwe watu fulani.

"Hati ya Uteuzi" ina maana ya hati za uteuzi
kama ilivyoolezwa katika kifungu cha 5
cha Sheria hii.

"Kiapo cha Uaminifu" ina maana ya kiapo au
tamko lililofanywa na mtu alieteuliwa kushika
wadhifa fulani ulioolezwa katika hati ya
uteuzi na inajumuisha viapo vyengine vitavyo
kuwa ni lazima kwa utendaji wa kazi hiyo.

"Waziri" ina maana ya Waziri ambae kwa wakati
huu anashughulikia mambo ya Sheria.

"Katiba" ina maana ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

"Idara Maalum" ina maana ya Idara Maalum kama zilivyoanzishwa na Katiba.

Nani anae-takiwa kula kiapo cha Uaminifu.

3.(1) Viapo vya uaminifu vitafanywa na watu wafuataao:-

- (a) Rais
- (b) Waziri Kiongozi
- (c) Jaji Mkuu na Majaji wa Mahkama Kuu
- (d) Waziri na Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi
- (e) Naib Waziri
- (f) Mwanasheria Mkuu
- (g) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi
- (h) Spika wa Baraza la Wawakilishi
- (i) Katibu wa Baraza la Wawakilishi
- (j) Katibu Mkuu
- (k) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
- (l) Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya na
- (m) Mtu mwengine ye yote anaetarajiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa Katiba au Sheria nyengine yo yote.

(2) Mbali na watu waliotajwa katika kijifungu cha (1) cha kifungu hichi watu wafuatao pia watapaswa kula viapo vya Uaminifu na viapo vya utendaji wa kazi:-

- (a) Kadhi Mkuu,
- (b) Wakuu wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi,
- (c) Washauri wa Rais,
- (d) Katibu wa Rais na
- (e) Afisa Tawala Mkoa na Wilaya.

(3) Mtu ye yote aliyetajwa katika kijifungu cha (1) au (2) cha kifungu hichi hatoanza kazi yake mpaka kwanza ale kiapo chengine cho chote cha utendaji wa kazi yake kama inavyoonyesha katika Jadweli ya kwanza ya Sheria hii.

(4) Viapo vyote vilivyoainishwa katika kifungu hichi vitatekelezwa katika fomu na namna ambayo Waziri ataitengeneza.

Jani
ataeapisha
Kiapo vya
Uaminifu.

4. Mteuzi wa wadhifa, au Afisa aliemuwakilisha kwa niaba yake ndie ataaeapisha kiapo cha Uaminifu. Itajui likana kwamba kiapo cha Uaminifu kwa Rais, Waziri Kiongozi, Spika wa Baraza la Wawakilishi na Jaji Mkuu vitaapishwa kwa mpangilio na Jaji Mkuu, Rais, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na Rais tu.

Hati za Uteuzi.

5.(1) Pale ambapo mtu amekula kiapo cha Uaminifu mteuzi au mtu anaemuwakilisha, kwa kadiri inavyokuwa atamkabidhi mtu alieteuliwa na ambae ameshakula kiapo hicho, hati ya uteuzi ikionesha:-

- (a) Tarehe ya kuanzia uteuzi wake huo;
- (b) Haki zake na
- (c) Kitu chengine cho chote ambacho mteuzi atahisi ni vizuri kukitaja.

(2) Hati za uteuzi zitakuwa katika namna ilioelezwa katika Jadweli ya Pili ya Sheria hii.

Kamuni.

6.(1) Waziri anaweza kuweka Kamuni ambazo zitasaidia kufanikisha lengo la Sheria hii.

(2) Waziri anaweza kuongeza orodha ya watu wanaopaswa kula viapo vya Uaminifu na vya Utendaji wa kazi kwa kutoa notisi katika Gazeti la Serikali.

Kihalalisha
viapo
vivilvyopita.

7. Viapo vyote vya Uaminifu vilivyoapwa na watu mbali mbali kabla ya kutumika Sheria hii vitahesabika kuwa ni viapo vya kihalali kama kwamba **vimeapwa** chini ya Sheria hii.

JEDWELI NAM. I
1. KIAPO CHA RAIS
KIAPO CHA UAMINIFU
(CHINI YA KIFUNGU 3(1)(a))

MIMI naapa
Kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakuwa mwaminifu kwa
Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi,
nitailinda, nitaitii na kuitetea Katiba ya Zanzibar na watu
wake kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaide.

(2) Kiazo cha Rais wa Zanzibar,
na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

MIMI nitaitekeleza
kazi zangu za Urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
kwa uaminifu, na uadilifu, na kutimiza wajibu wangu kwa moyo mkunjufu
na kwamba nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba na Sheria
nikiongozwa na Haki, Mila na Desturi za Zanzibar, bila ya kushawishiwa,
Woga, Upendeleo au Chuki.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaide.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa

....., Zanzibar
leo tarehe 198

SAHIHI
Ameapa mbele yangu leo
Tarehe

SAHIHI
JAJI MKUU ZANZIBAR

2. KIAPO CHA WAZIRI KIONGOZI
1. KIAPO CHA UAMINIFU
(CHINI YA KIFUNGU 3(1)(b))

MIMI naapa
Kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar
ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia
kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda, nitaitii na
kuitetea Katiba ya Zanzibar na watu wake kwa mujibu wa Sheria
ilivyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.
(2) Kiapo cha Utendaji wa Kazi za
Waziri Kiongozi na Serikali
ya Mapinduzi ya Zanzibar.

MIMI hapa naapa
kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar katika Utendaji wangu na Uwaziri Kiongozi
na kwamba wakati wote nitamshauri kwa Hekima na Uaminifu Rais
wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kwa vyo vyote
sitotoa Siri za Serikali ya Zanzibar.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.
Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI
Ameapa mbele yangu leo
Tarehe

SAHIHI
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA
MAPINDUZI

3. KIAPO CHA MAJAJI
1. KIAPO CHA UAMINIFU
(CHINI YA KIFUNGU 3 (1)(c))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar na kuitumikia kwa
moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitalinda na
kuitetea Katiba ya Chama cha Mapinduzi, Katiba ya Zanzibar,
na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UJAJI WA MAHKAMA KUU YA ZANZIBAR

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia kwa uaminifu na kwa moyo thabiti Zanzibar
na watu wake na nitakua mtii kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti
wa Baraza la Mapinduzi katika kazi yangu ya Ujaji Mkuu/Jaji
wa Mahkama Kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na nitafanya
haki kwa mujibu wa Katiba ya Chama cha Mapinduzi, Katiba ya
Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila
kushawishiwa, Hofu, Upendeleo au Chuiki.

(3) KIAPO CHA KULINDA SIRI

MIMI naapa
kwamba katika kazi yangu ya Uhakimu na Serikali ya Zanzibar
kwa vyo vyote vile sitatoa siri ambazo nitazijua katika kazi
zangu isipokua katika wajibu wa kazi hizo au kwa idhini ya
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula viapo hivi hapa Zanzibar
..... leo tarehe

Ameapa mbele yangu leo tarehe

RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

4. KIAPO CHA WAJUMBE WA BARAZA LA MAPINDUZI

1. KIAPO CHA UAMINIFU

CHINI YA KIFUNGU 3(1)(a)

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni Sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu
wote na kwamba nitailinda, nitaihifadhi na kuitetea Katiba
ya Zanzibar na watu wake kwa mujibu wa Sheria iliyyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WAJUMBE
WA BARAZA LA MAPINDUZI

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema kwa moyo thabiti Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa kazi zangu za
Ujumbe wa Baraza la Mapinduzi na kwamba wakati wo wote
nitamshauri kwa hekima na uaminifu Mwenyekiti wa Baraza la
Mapinduzi na kwa vyo vyote vile sitotoa siri za Baraza la
Mapinduzi.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA
BARAZA LA MAPINDUZI

4B. KIAPO CHA WAZIRI WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA
ZANZIBAR

(1) KIAPO CHA UAMINIFU
(CHINI YA KIFUNGU 3(1)(a))

MIMI naapa
kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakua muaminifu kwa Zanzibar
ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Miungano wa Tanzania na kuitumikia
kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda, nitaitii
na kuitetea Katiba ya Zanzibar na watu wake kwa mujibu wa Sheria
iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WAZIRI WA
SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema kwa moyo thabiti Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar katika kazi zangu za Uwaziri katika
Wizara ya na kwamba wakati
wote nitamshauri kwa hekima na uaminifu Rais wa Zanzibar na
Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kwa vyo vyote vile
sitatoa siri za Serikali ya Zanzibar.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHITHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe.....

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

5. KIAPO CHA NAIB WAZIRI
1. KIAPO CHA UAMINIFU
CHINI YA KIFUNGU NAM. 3(1)(e)

MIMI naapa
kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakua muaminifu kwa
Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi,
nitailinda, nitaitii na kuitekeleza Katiba ya Zanzibar na
watu wake kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTEKELEZAJI WA KAZI CHA
NAIBU WAZIRI

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema kwa moyo thabiti Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar katika kazi zangu za utekelezaji za
Unaibu Waziri katika Wizara ya
na kwamba wakati ~~wote~~ nitamshauri kwa hekima na uaminifu
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na
kwa vyo vyote vile sitatoa siri za Serikali ya Zanzibar.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

6. KIAPO CHA MWANASHERIA MKUU

(1) KIAPO CHA UAMINIFU

(CHINI YA KIFUNGU NAM. 3(1)(f))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu
wote na kwamba, nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba
ya Chama cha Mapinduzi, Katiba ya Zanzibar na Katiba ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MWANASHERIA
MKUU

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia kwa uaminifu na moyo thabiti Serikali ya
Mapinduzi katika kazi za Mwanasheria Mkuu na nitaihami vyema
Kisheria Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa
Katiba ya Chama Cha Mapinduzi, Katiba ya Zanzibar na Katiba
ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya kushawishiwa, hofu,
upendeleo au chuki.

(3) KIAPO CHA KULINDA SIRI

MIMI naapa
kwamba katika kazi yangu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar kwa vyo vyote vile sitatoa siri ambazo
nitazijua katika kazi yangu isipokuwa katika kutimiza wajibu
wa kazi hizo au kwa idhini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa
Baraza la Mapinduzi.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula viapo hivi hapa Zanzibar
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

7. KIAPO CHA MJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

(1) KIAPO CHA UAMINIFU

(CHINI YA KIFUNGU NAM. 3 (1) (g))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi zangu za Uwakilishi,
na kuitumikia kwa moyo wangu wote, na kwamba nitaihifadhi na
kuitetea Katiba ya Chama cha Mapinduzi, Katiba ya Zanzibar kwa
mujibu wa Sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Kiapo hichi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
SPIKA WA BARAZA LA WAWAKILISHI

8. KIAPO CHA SPIKA WA BARAZA LA WAWAKILISHI

(1) KIAPO CHA UAMINIFU

(CHINI YA KIFUNGU NAM. 3(1)(h)

KIAPO CHA UTENDAJI KAZI ZA USPIKA

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Chama cha Mapinduzi na kwa
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kazi zangu za Uspika
na kuitumikia kwa moyo wangu wote, na kwamba nitaihifadhi,
nitailinda na nitaitetea Katiba ya Chama, Katiba ya Zanzibar
na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

.....
SPIKA

Ameapishwa na kutia sahihi mbele yangu.

.....
KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI

Tarehe19....

9. KIAPO CHA KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI

(1) KIAPO CHA UAMINIFU

(CHINI YA KIFUNGU 3 (1)(a))

MIMI naapa
kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakuwa mwaminifu kwa
Serikali ya Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote, na kwamba
nitaihifadhi, nitaitii na kuitekeleza Katiba ya Zanzibar na
watu wake kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTENDAJI KAZI ZA KATIBU WA
BARAZA LA WAWAKILISHI

MIMI naapa
kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitaitumikia kwa uaminifu
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kazi zangu za
ukatibu wa Baraza la Wawakilishi na kwa vyo vyote vile
sitatoa siri za Serikali ya Zanzibar.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHITHI

Ameapa mbele yangu leo

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

10. KIAPO CHA UTEKELEZAJI KAZI ZA UDHIBITI WA
UKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

(1) KIAPO CHA UAMINIFU
(CHINI YA KIFUNGU NAM. 3(1)(k))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri
ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote na
kwamba nitaihifadhi, na kuitetea Katiba kwa mujibu wa sheria
iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTEKELEZAJI KAZI ZA MDHIBITI NA
MKAGUKI MKUU WA SERIKALI

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa
Baraza la Mapinduzi katika kazi yangu ya udhibiti na ukaguzi
mkuu wa hesabu za Serikali na kwa vyo vyote vile sitatoa siri
za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

11(A). KIAPO CHA KATIBU MKUU/NAIBU KATIBU MKUU

(1) KIAPO CHA UAMINIFU

(CHINI YA KIFUNGU 3(1)(j))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo
wangu wote na kwamba nitajihifadhi, nitailinda, na kuitetea
kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTENDAJI WA KAZI CHA UKATIBU MKUU

NA NAIBU KATIBU MKUU

WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia kwa uaminifu Serikali ya Mapinduzi ya
Zanzibar katika kazi za Ukatibu/Mkuu/NKM katika Wizara ya
..... na kwa vyo vyote
vile sitotoa siri ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha nimekula viapo hivi hapa.....
leo tarehe

SAHIFI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

11B. KIAPO CHA KATIBU/NAIBU KATIBU WA BARAZA
LA MAPINDUZI
(1) KIAPO CHA UAMINIFU
(CHINI YA KIFUNGU 3 (1)(j))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu
wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda, na kuitetea kwa
mujibu wa sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTENDAJI KAZI YA KATIBU/
NAIBU KATIBU WA BARAZA LA MAPINDUZI

MIMI naapa
kwamba isipokuwa kwa idhini ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la
Mapinduzi, sitotoa siri ya Baraza la Mapinduzi au taarifa au
habari yoyote niliyopewa Kama ni Katibu/Naibu Katibu wa Baraza
la Mapinduzi au kitu cho chote nitachokijua kutokana na kazi
yangu ya Katibu/Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi, lakini
nitatumikia vyema na kwa moyo thabiti kazi yangu ya Ukatibu/
Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIDI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

12. KIAPO CHA MKUU WA MKOA

(1) KIAPO CHA UAMINIFU

(KIFUNGU NAM. 3 (1) (1))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba
nitaihifadhi, na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania, Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Chama Cha Mapinduzi
kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu Unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTENDAJI WA KAZI CHA
MKUU WA MKOA

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Zanzibar na
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi zangu za Mkuu
wa Mkoaa, na wakati wote nitamshauri kwa hekima na uaminifu
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la
Zanzibar, na kwa vyo vyote vile sitotoa siri za Serikali.

Nakuomba Mwenyezi Mungu Unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

12B. KIAPO CHA MKUU WA WILAYA

(1) KIAPO CHA UAMINIFU

CHINI YA KIFUNGU NAM. 3(1)(1)

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu
wote na kwamba nitainihifadhi na kuitetea Katiba ya Zanzibar
kwa Mujibu wa Sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTENDAJI WA KAZI CHA MKUU WA WILAYA

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema kwa moyo thabiti Zanzibar katika
kazi zangu za Mkuu wa Wilaya na kwa wakati wote nitamshauri
kwa hekima Mkuu wa Mkoa na kwa vyo vyote vile sitat&a siri
za Serikali.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
leo tarehe

SAHIDI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
MKUU WA MKOA

MKOA WA /Unguja/Pemba

13. KIAPO CHA KADHI MKUU
KIAPO CHA UAMINIFU
(CHINI YA KIFUNGU 3 (2)(a))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar na kuitumikia kwa
moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na
kuitetea Katiba ya Chama cha Mapinduzi, Katiba ya Zanzibar
na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Nakuomba Mwenyezzi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA KADHI MKUU WA ZANZIBAR

MIMI naapa
kwamba nitatumikia kwa uaminifu na kwa moyo thabiti Zanzibar
na watu wake na nitakua mtii kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti
wa Baraza la Mapinduzi katika kazi yangu na Ukadhi Mkuu na
nitafanya haki kwa mujibu wa Sheria ya Kiislam, Katiba ya
Zanzibar na Sheria nyengine zilizowekwa bila ya kushawishiwa,
hofu, upendeleo au chuki.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa leo mbele yangu tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

14. KIAPO CHA UTEKELEZAJI KAZI ZA MKUU WA
IDARA MAALUM
KIAPO CHA UTII
(CHINI YA KIFUNGU 3(2)(b))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar na kuitumikia kwa moyo
wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba
ya Chama Cha Mapinduzi, Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri
ya Muungano wa Tanzania.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTEKELEZAJI KAZI

MIMI Mkuu wa Kikosi
cha naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Rais na Serikali yake na kwamba
nitamatumikia Rais kwa moyo wote kwa muda wote nitakuwa katika
Kikosi na kwamba nitatii, nitaheshimu na nitatekeleza Sheria,
Amri na Kamuni zote za Serikali pameja na kutii na kutekeleza
Amri na Maagizo mengine nitayopewa na Rais ikiwa ni Mkuu wa
Idara Maalum.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekuia Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa leo mbele yangu tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITTI WA BARAZA LA MAPINDUZI

15. KIAPO CHA MSHAURI WA RAIS

1. KIAPO CHA UAMINIFU

(CHINI YA KIFUNGU 3 (2)(e))

MIMI naapa
kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu
wote na kwamba nitailinda, nitaihifadhi na kuitetea Katiba
ya Zanzibar na watu wake kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MSHAURI WA
RAIS WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema kwa moyo thabiti Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa kazi zangu za
Kumshauri Rais wa Zanzibar na kwamba wakati wo wote nitamshauri
kwa hekima na uaminifu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa
Baraza la Mapinduzi na kwa vyo vyote vile sitatoa siri za
Serikali.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHITHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

16. KIAPO CHA KATIBU WA RAIS

1. KIAPO CHA UAMINIFU

(CHINI YA KIFUNGU NAM. 3(2)(a))

MIMI naapa
kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar
ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia
kwa moyo wangu wote, na kwamba nitaihifadhi, nitailinda, nitaitii
na kuitekeleza Katiba ya Zanzibar na watu wake kwa mujibu wa
Sheria iliyowekwa.

NAKUOMBA MWENYEZI MUNGU UNISAIDIE.

(2) KIAPO CHA UTENDAJI WA KAZI ZA KATIBU WA RAIS

MIMI naapa
kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitatumikia kwa uaminifu
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kazi za Ukatibu wa
Rais na kwa vyo vyote vile sitotoa siri za Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar.

NAKUOMBA MWENYEZI MUNGU UNISAIDIE.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIHI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

17. KIAPO CHA UTENDAJI KAZI CHA AFISA
TAWALA MKOA/WILAYA
(CHINI YA KIFUNGU 3(2)(e))

MIMI naapa
kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Zanzibar
katika kazi zangu za Afisa Tawala na kua wakati we wote
nitamshauri kwa hekima Mkuu wa Mkoo/Wilaya na kwa vyo vyote
vile sitata siri za Serikali.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

(2) KIAPO CHA AFISA TAWALA WA MKOA/WILAYA
KIAPO CHA UAMINIFU

MIMI naapa
kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo
wangu wote na kwamba nitaihifadhi na kuitetea Katiba ya
Zanzibar kwa mujibu wa sheria iliowekwa.

Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie.

Nahakikisha kwamba nimekula Viapo hivi hapa
..... leo tarehe

SAHIFI

Ameapa mbele yangu leo tarehe

.....

MKUU WA MKOA

Mkoo wa Unguja/Pemba.

JADWELET NAMBA MBILI
KUTEULIWA KUWA
(CHINI YA KIFUNGU NAMBA 5)

Kwa

Salaam:

KWA UWEZO NA MAMILAKA NILIYONAYO

Chini ya Kifungu cha Katiba, NINAKUTEUWA
WEWE kuwa
.....
kuanzia tarehe mwezi wa
mwaka NA NINAKUAGIZA uzitekeleze kazi zote za
..... pamoja na madaraka
mengine yote ambayo utapewa mara kwa mara kufuata sheria, kwa
uaminifu na juhudii.


Kwa kuthibitisha, nimetia sahihi yangu na muhuri
wa Serikali hii leo tarehe 19

.....
RAIS WA ZANZIBAR NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

ZANZIBAR,

Tarehe 19

Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 21 Januari,
1986.


Salum Mzee
KAIMU KATIBU WA
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR.

